ENERGY AND WATER UTILITIES REGULATORY AUTHORITY
RECEIVED
19 NOV 2021
EASTERN ZONE

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI

(EWURA)

MALALAMIKO NAMBA. SN.71/135/119

DP AND COMPANY LIMITED..... MLALAMIKAJI

MWAKILISHI: MICHAEL DP MALAMSHA

DHIDI YA

TANESCO..... MLALAMIKIWA

TUZO YA MAKUBALIANO

(Imetolewa na Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kupitia waraka wake Na. 20 wa tarehe 3 Novemba, 2021)

1.0 Maelezo ya Awali

Mnamo tarehe 14 Juni 2021, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa Bw. Michael DP Malamsha, mwakilishi wa kampuni ya DP and Company Limited ("Mlalamikaji") wa Kinondoni mkoa wa Dar es Salaam dhidi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ("Mlalamikiwa"). Mlalamikaji analalamikia deni la umeme katika dira yake ya LUKU kiasi cha TZS 7,080,408.31, deni ambalo linahusishwa na mteja mwenye jina la Adriano Katamah ambaye Mlalamikaji anakana kumtambua.

Mlalamikaji anaeleza kuwa, mnamo tarehe 6 Mei 2021, alifanya manunuzi ya umeme wa kuendesha biashara yake akashangazwa na makato ya uniti za umeme alizonunua bila taarifa. Katika kufuatilia tatizo hili kwenye ofisi za Mlalamikiwa, alitaarifiwa kuwa dira ya Luku anayotumia ina deni la nyuma kiasi cha TZS 7,080,408.31 ("deni bishaniwa"). Mlalamikaji alifanya jitihada za

kutafuta suluhu ikiwemo kumwandikia barua Mlalamikiwa mnamo tarehe 25 Mei 2021 akimweleza kuwa hatambui deni hilo. Ilipofika tarehe 2 Juni 2021, Mlalamikaji alijibu barua na kumtaarifu Mlalamikiwa kuwa deni hilo linatokana na aliekuwa mteja wake Bw. Adriano Katamah mwenye mita namba 51041816 ambae Mlalamikiwa anasadiki kuwa Mlalamikaji alinunua eneo kwake.

Mlalamikaji alileta malalamiko yake EWURA na kuiomba Mamlaka imwamuru Mlalamikiwa:

a) kufuta deni hilo kwa kuwa halitambui na pia hamtambui Bw. Adriano Katamah kwa namna yeyote ile;
b) kurudishiwa uniti zilizokatwa baada ya manunuzi ya umeme;
c) kusitisha makato ya uniti kwenye manunuzi ya umeme wakati shauri linaendelea kusikilizwa kwani ni mzigo mkubwa sana kwa kampuni; na
d) Mlalamikiwa kuwajibika na gharama zozote endapo kampuni itapata hasara ya aina yeyote katika kufuatilia deni hili.

Baada ya kupokea malalamiko ya Bw. Michael DP Malamsha, Mamlaka (EWURA) tarehe 16 Juni 2021, ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuleta waraka wa utetezi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa kanuni ya 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Taratibu za Kutatua Migogoro '*Rule 7 (1) of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Complaints Handling Procedure) Rules, GN No. 428/2020*'.

Mlalamikiwa alileta utetezi wake tarehe 06 Julai 2021 akieleza kwamba anapinga maelezo ya kipengele cha 3 cha malalamiko na anaeleza zaidi kuwa Mlalamikaji ni mteja wake na alikua akipata huduma ya umeme kwa kutumia dira ya kusoma namba 51016260 yenye jina la V.H Assenga na dira namba 51015650 yenye jina la Damas Malamsha. Mlalamikiwa aneleza Zaidi kuwa baadae Mlalamikaji aliongeza eneo kwa kununua eneo lililokuwa karibu na dira tajwa hapo juu. Eneo lililonunuliwa lilikuwa linahudumiwa na dira namba 51016259 kwa jina la Mnyamani Ngomani na namba 51041816 kwa jina la Adriano Katamah. Mllamikaji anadai kuwa dira namba 51016259 na dira namba 51041816 zilikuwa na deni ambalo jumla yake ni TZS 7,080,408.31. Baada ya

Mlalamikiwa kugundua kwamba eneo hilo lilikuwa limenunuliwa na Mlalamikaji deni hilo lilihamishiwa kwenye dira ya Mlalamikaji.

Kikao cha kwanza cha usuluhishi kilifanyika tarehe 27 Julai 2021, katika Ofisi za EWURA Kanda ya Mashariki ambapo wadaawa hawakufikia muafaka na shauri likapelekwa kwa hatua ya kusikilizwa ambapo shauri lilipokuja kwa ajili ya kusikilizwa mnamo tarehe 7 Septemba 2021 Mlalamikiwa aliomba shauri lirejeshwe tena katika kikao cha usuluhishi ambapo ombi lake lilikubaliwa.

Kikao cha pili cha usuluhishi kilifanyika tarehe 17 Septemba 2021, katika ofisi za EWURA Kanda ya Mashariki. Mwisho wa kikao cha usuluhishi wadaawa walikubaliana yafuatayo:

(i) Mlalamikiwa atafuta deni lote la TZS 7,080,408.31 na utekelezaji wake utakamilika kufikia Ijumaa tarehe 24 Septemba 2021;
(ii) Mlalamikiwa atarejesha pesa zote zilizokatwa kulipia deni bishaniwa, pesa ambazo zilikatwa kwa kila manunuzi ya umeme aliyofanya Mlalamikaji kuanzia tarehe 1 Mei 2021. Marejesho hayo yatafanyika ifikapo Ijumaa tarehe 24 Septemba 2021; na
(iii) Mlalamikaji ameondoa nafuu namba 4 ya madai ya gharama zitakazojitokeza katika shauri hili kama alivyoomba katika fomu ya malalamiko.

Makubaliano haya yamewekwa kwenye maandishi kama inavyoainishwa kwenye Kanuni ya 14(4) ya Kanuni za EWURA za Taratibu za Kutatua Migogoro T.S namba 428/2020 '*Rule 14 (4) of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Complaints Handling Procedure) Rules, GN No. 428/2020'* na kama ilivyoainishwa kwenye fomu ya muafaka.

2.0 Makubaliano

Pande zote mbili zimefikia muafaka kama ifuatavyo:

(i) Mlalamikiwa atafuta deni lote la TZS 7,080,408.31 na utekelezaji wake utakamilika kufikia Ijumaa tarehe 24 Septemba 2021;

(ii) Mlalamikiwa atarejesha pesa zote zilizokatwa kwa ajili ya kulipia deni bishaniwa , pesa ambazo zilikatwa katika manunuzi ya umeme aliyofanya Mlalamikaji kuanzia tarehe 1 Mei 2021. Marejesho hayo yatafanyika ifikapo Ijumaa tarehe 24 Septemba 2021; na

(iii) Mlalamikaji ameondoa nafuu namba 4 ya madai ya gharama zitakazojitokeza katika shauri hili kama alivyoomba katika fomu ya malalamiko.

na kwa mujibu wa kanuni ya 14(5) ya Kanuni za EWURA za Taratibu za Kutatua Migogoro T.S namba 428/2020, makubaliano haya yameandikishwa kama Tuzo ya Mamlaka. Kila upande utabeba gharama zake katika shauri hili.

IMETOLEWA KWA LAKIRI ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Dodoma tarehe 3 Novemba, 2021.

.....

KAPWETE LEAH JOHN
KATIBU WA BODI